



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**



## **TAARIFA KWA UMMA**

Dodoma 19 Novemba 2025

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bw. Eliakimu Maswi, amewataka watumishi wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kuongeza ubunifu na kutumia maarifa mapya katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku, ili kuongeza ufanisi na kuendana na mabadiliko ya kiutendaji ndani ya Serikali.

Maswi alitoa wito huo tarehe 19 .11.2025 wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika katika Hoteli ya Sanaan, jijini Dodoma, Kikao kilichowakutanisha wajumbe wa Baraza la wafanyakazi watumishi mbalimbali kutoka ngazi mbalimbali za TUGHE Taifa na ngazi ya Mkoa.

Akizungumza wakati wa ufunguzi huo, Maswi alisema Tume ina nafasi muhimu katika uimarishaji wa misingi ya utawala bora, hivyo watumishi wanapaswa kuongeza ubunifu katika utatuzi wa changamoto, utafiti, na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Aliongeza kuwa ubunifu si jukumu la idara fulani tu, bali ni wajibu wa kila mtumishi, kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu. Alisisitiza kuwa Serikali inategemea mawazo mapya kutoka kwa watumishi wake ili kuharakisha maboresho ya mifumo ya sheria na haki.

**Bashiri S. Juma**  
**Kitengo cha Mawasiliono Serikalini**

**Chuo Kikuu cha Dodoma, Barabara ya Mkalama, Jengo la Taaluma Na.1, S.L.P. 1718, Dodoma.**  
**Tovuti: [www.lrct@lrct.go.tz](http://www.lrct@lrct.go.tz); Barua pepe: [lrct@lrct.go.tz](mailto:lrct@lrct.go.tz); Simu: +255734 356685/6**